

PATA KUJUA UKWELI.

CHANJO INATOLEWA BILA MALIPO KWA WATU WOTE.



Lakini hakikisha na uulize ikiwa kuna gharama zingine za ziada za kupewa chanjo.

- Hakuna mtu anaweza kunyimwa chanjo ikiwa hawawezi kulipa ada ya kupewa chanjo.
- Mara tu chanjo zinapopatikana kwa wingi, mtu yeyote anaweza kupata chanjo bila kujali hali ya uhamaji.
- Kila mtu anaweza kuchanjwa wakati ni zamu yao.

Chanjo hukulinda kutokana na kuambukizwa COVID-19.

- Ikiwa bado utaambukizwa COVID baada ya kupewa chanjo, chanjo hukulinda usiwe mgonjwa sana.
- Hata ikiwa ulikuwa na COVID-19, bado unapaswa kupewa chanjo.
- Bado haijulikana mtu atalindwa kwa muda gani kabla ya kuugua tena kutokana na COVID-19.



Chanjo za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi. Chanjo HAIWEZI kukuambukiza COVID-19.

- Ni salama kupata chanjo kuliko kuambukizwa COVID-19.
- Mamilioni ya watu wamechanjwa kwa usalama.
- Katika historia ya Marekani, hakuna chanjo nyingine ambayo usalama wake umechunguzwa kiasi hiki.
- Chanjo imethibitishwa kuwa salama kwa maelfu ya watu, wakiwemo watu wa rangi, kabila na umri tofauti tofauti.
- Chanjo ya COVID-19 haibadilishi DNA yako.

ATHARI NI ZA KAWAIDA.

Athari HAZIMAANISHI umeambukizwa COVID-19.

- Athari humaanisha kuwa chanjo inafunza mwili wako jinsi ya kupigana na COVID-19.
- Athari zinaweza kujumuisha:
 - Maumivu au kuvimba kwenye sehemu ya mkono ambapo ulidungwa sindano ya chanjo.
 - Maumivu ya kichwa, baridi au homa ya joto.
- Ukijihisi mgonjwa, pumzika kwa siku chache hadi uhisi nafuu kisha urejee kazini.
- Utahitaji kukaa kwa muda wa dakika 15–30 baada ya chanjo yako ili uhakikishe huna mzio.



Hakuna ushahidi kwamba chanjo zinasababisha shida za uzazi.

Wanawake wajawazito wanapaswa kuzungumza na daktari wao kuhusu kuchanjwa.

Chanjo zingine zinahitaji sindano mbili ilhali zingine zinahitaji sindano moja tu. Aina hizi mbili za chanjo ni salama na zenye ufanisi.

Kwa chanjo ambazo zinahitaji sindano **mbili**:

- Sindano ya kwanza hutayarisha mwili wako.
- Sindano ya pili hupeanwa wiki kadhaa baadaye ili kuhakikisha uko na ulinzi kamili.
- Ni muhimu uweze kupata sindano zote mbili ili ulindwe vikamilifu.

Chanjo HAZINA

- Vihifadhi
- Mayai
- Bidhaa za nguruwe
- Gelatini
- Lateksi
- Virusi vyovyote hai vya COVID-19

KAA SALAMA BAADA YA KUCHANJWA.

Kwa wakati huu, wataalamu hawajui chanjo itakulinda kwa muda gani. Hata baada ya kupata chanjo, endelea:



Kuvaa maski.



Kuhakikisha hukaribiani na watu.



Kunawa mikono yako mara kwa mara.



Kusafisha sehemu zinazoguswa mara kwa mara.



NRC-RIM

National Resource Center for
Refugees, Immigrants, and Migrants

Kwa maelezo zaidi: cdc.gov/coronavirus